# Tahariri

Makala katika Toleo hili la 2 la Juzuu la 88 la mwaka 2025 ni maalumu kuhusu fasihi na mazingira. Makala hizi ni matokeo ya Kongamano la Mashariki la 7 la Taaluma za Fasihi na Utamaduni lililofanyika katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuanzia tarehe 21-23 Agosti 2025. Kongamano hili hufanyika kwa ushirikiano wa wadau wa fasihi na utamaduni katika Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, wengi wao wakitokea katika idara za fasihi kwa Kiingereza katika taasisi za elimu ya juu. Kongamano hili hufanyika kwa zamu kutoka nchi moja hadi nyingine katika eneo la Afrika Mashariki. Katika Kongamano hilo, kulikuwa na jopo la Kiswahili ambapo lugha ya mawasilisho ilikuwa Kiswahili na maudhui yake yalihusu fasihi na mazingira kwa ujumla. Kwa mara ya kwanza Kongamano hilo lilitoa fursa kwa wadau wa Kiswahili kuwasilisha mada zao kama sehemu ya Kongamano la Mashariki. Tunaishukuru sana Kamati ya maandalizi ya Kongamano hilo kwa kutoa nafasi ya mawasilisho kwa Kiswahili.

Toleo hili lina makala zilizowasilishwa katika Kongamano hilo na nyingine ambazo hazikuwasilishwa wakati huo. Ili kumrahisishia msomaji wa fasihi na mazingira, makala mbalimbali zinazohusu mazingira zilizowasilishwa kwa ajili ya kufikiriwa kuchapishwa katika *Jarida la Kiswahili*, zimejumuishwa katika toleo hili. Tunatumaini kwamba msomaji wa makala zilizochapishwa katika toleo hili atafurahia michango ya waandishi iliyolenga maeneo mbalimbali kama vile riwaya, semi, simulizi kadha wa kadha za mdomo, matambiko na ushairi. Hata hivyo, kutokana na umuhimu wa suala la mazingira, tunaendelea kuwasihi waandishi, waendelee kufanya tafiti kuhusu eneo hili na kututumia miswada yao. Endapo itapatikana ya kutosheleza mahitaji ya toleo lingine kuhusu mazingira, litaandaliwa.

Ufuatao ni muhtasari wa makala zilizochapishwa katika toleo hili. Akifanya uchambuzi wa riwaya ya *Nakuruto* ya Clara Momanyi, Lina Akaka anazua mjadala kuhusu namna unyonyaji wa kibeberu unavyoathiri mazingira. Katika makala yenye kichwa, “Uchunguzi wa Ikolojia-Ubeberu katika Fasihi ya Kiswahili: Mfano wa Riwaya ya *Nakuruto* ya Clara Momanyi”, mwandishi anaeleza kuwa unyonyaji wa rasilimali unaoongozwa na ubeberu umechangia katika uharibifu wa mazingira. Akaka anaeleza kuwa sifa za kibeberu, yaani uchoyo, ubinafsi na tamaa ya kujinufaisha kutokana na maliasili ambayo inajumuisha vyanzo vya maji, milima, udongo, madini pamoja na miti, zimechangia kuharibu dunia na kuhatarisha maisha katika sayari hii.

Kwa upande mwingine, makala yenye kichwa, “Miti kama Elementi ya Udhibiti wa Miundomsingi ya Kijani katika Diwani Teule za Ushairi wa Kiswahili” iliyoandikwa na Mwaniki Mugwe, Rayya Timammy na Omboga Zaja imejikita katika ushairi ambapo inabainisha namna ushairi unavyojadili suala la miti kama kipengele kimojawapo cha miundomsingi ya kijani. Wakitumia diwani za *Kina cha Maisha* (Mohammed, 1984), *Jicho la Ndani* (Mohammed, 2002), *Msimu wa Tisa*

(Mberia, 2007) na *Doa* (Mberia, 2018), waandishi hawa wanaeleza umuhimu wa miti katika sura mbalimbali kuanzia kwa binadamu ambayo hutumika kama vile chakula na dawa hadi katika umuhimu wa kutunza mazingira kwa ujumla.

Akijadili kuhusu "Nafasi ya Rasilimali Jadi katika Uhifadhi na Utunzaji wa Mazingira", Doroth Mosha anaeleza kuwa rasilimali jadi, ambazo ni vipengele vya fasihi simulizi kama vile semi, miviga, hadithi, maigizo na ushairi simulizi zilizokuwapo tangu kale katika mfumo wa maisha ya mwanadamu, zina mchango mkubwa katika utunzaji wa mazingira kwa namna mbalimbali, vikiwamo visasili vinavyohusu maeneo muhimu yasiyopaswa kuharibiwa. Aidha, kuna shirikina ambazo zina makatazo kadha wa kadha yanayosaidia kutunza mazingira. Rasilimalijadi hizi zimefumbata elimu jadi ya kuhifadhi mazingira. Hata hivyo, pamoja na umuhimu wake zinaendelea kufifia na pengine kupotea endapo hakutakuwa na mikakati ya kuziendeleza.

Shani Omari Mchepange anajadili namna semi za Kiswahili zilivyofumbata sura mbalimbali za mazingira. Katika makala yake yenye kichwa, "Maarifa ya Kiikolojia na Kijamii kutoka katika Methali za Kiswahili Zinazotaja Mimea", anaeleza kwamba methali hutoa maarifa mbalimbali kuhusu ikolojia kwa uchangamani wake wote, yaani maarifa kuhusu kutegemeana kwa viumbe mbalimbali, shughuli za binadamu, tabia za viumbe na changamoto mbalimbali za kimazingira pamoja harakati za utunzaji wake huku suala la uhusiano wa ikolojia na maarifa mengine anuwai likifafanuliwa. Kwa ujumla, methali zinaakisi mazingira ya jamii itumiayo semi husika.

Akijadili matini ya matambiko ya Wapangwa, Winne S. Mtega, anaeleza namna itikadi ya ardhi inavyosaidia katika utunzaji wa mazingira. Katika makala yake, "Itikadi ya Ardhi katika Miviga kama Mhimili wa Utunzaji Mazingira: Mifano kutoka Ushairi wa Matambiko ya Wapangwa", mwandishi anaeleza kwamba itikadi ya ardhi imedhihirika katika matambiko na kudokeza falsafa ya ardhi kuwa chanzo na asili ya maisha. Kwa maneno mengine, ardhi ni utambulisho wa jamii na chanzo cha uhai kwani chakula na maji hutokana na ardhi. Kutokana na umuhimu huo, itikadi ya ardhi huchochea mazingira kutunzwa.

Katika makala yenye kichwa, "Sitiari ya Bahari katika Ushairi wa Kiswahili: Mifano kutoka Nyimbo Teule za Muziki wa Dansi" Angelus Mnenuka na Neema Sway wanachambua dhana ya bahari inavyofafanuliwa vyema katika sitiari za bahari zinazopatikana katika nyimbo za muziki wa dansi. Katika makala hii, waandishi wanadai kuwa sitiari zinafumbata mila na desturi za jamii. Katika uchambuzi wao wa kikoa chanzi cha sitiari, wameonesha namna bahari inavyotazamwa kama sehemu hatari sana kwa maisha ya binadamu. Halikadhalika, wameonesha kuwa nyimbo hizohizo zinadokeza umuhimu bahari. Kwa hiyo, licha ya hatari zake, bahari ina umuhimu katika maisha ya jamii.

Katika makala yake yenye kichwa, "Simulizi ya *Chemichemi Bikuri* na Nafasi yake katika Utunzaji wa Mazingira", Geniva Kazinja anajadili namna simulizi ya *Chemichemi Bikuri* inavyosaidia kulinda maadili ya utunzaji wa mazingira

kutegemea imani za kiasili, masharti ya kijamii na vitisho vya kimitholojia ili kudhibiti uharibifu wa mazingira. Katika makala hii, mwandishi anadhihirisha kuwa katika jamii za Kiafrika, uhifadhi wa mazingira ulihusishwa moja kwa moja na uhai na ustawi wa jamii, kwani mazingira safi yalichukuliwa kuwa msingi wa uhusiano bora wa binadamu na ulimwengu.

Maudhui yaliyomo kwenye makala hizi yanatoa mchango anuwai katika uelewa wa masuala mbalimbali ya mazingira katika jamii na mbinu mbalimbali za utunzaji wa mazingira. Aidha, makala zinadokeza njia mbalimbali za uharibifu wa mazingira na athari zake zinazoweza kujitokeza hivi karibuni na zile zitakazojitokeza miaka kadhaa baadaye.

Wahariri, 2025